

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAISI – TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA NACHINGWEA**

SHULE YA SEKONDARI NAMIKANGO

S.L.P 115

NACHINGWEA

TAREHE.....

KUMB: Na.LD/NDC/S.3958/A.10/2020/2021

**MZAZI /MLEZI WA.....**

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA KIDATO CHA KWANZA KATIKA SHULE YA  
SEKONDARI NAMIKANGO**

1. Jumuiya ya Shule ya Sekondari Namikango inayofuraha ya kukujulisha kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga kidato cha Kwanza katika Shule ya Sekondari Namikango, mwaka wa masomo 2021. Hongera sana. Shule ya Sekondari Namikango inapatikana katika Kata ya Namikango umbali wa 1 km kutoka shule ya msingi Namikango na 1.2 km kutoka shule ya msingi Nangunde, mpakani mwa Kijiji cha Namikango "A" na Kijiji cha Nangunde barabara ya Namikango – Nangunde
2. Shule inafundisha masomo ya Uraia(Civics), Historia(History), Jiografia(Geography), Kiswahili, Lugha ya Kingereza(English Language), Kemia(Chemistry), Fizikia(Physics), Baolojia(Biology) na Hisabati(Basic Mathematics), masomo ya Bookkeeping na Commerce yanategemea kupatikana kwa walimu wa masomo hayo.
3. Muhula wa masomo utanza tarehe **11.01.2021** Mwanafunzi anatakiwa kuripoti shule tarehe **11.01.2021** Mwisho wa kuripoti ni tarehe **30.01.2021** Fika na mahitaji yote yaliyoanishwa.

Unakaribishwa sana tarajia kupata unachokijia kwa kuwa Mazingira ni rafiki sana  
Kwa Usomaji.

.....

**Hussein A. Rukuba**

**Mkuu wa Shule Namikango Sekondari**

**0717 740 240**

## **Kiambata namba 1**

### **MAHITAJI YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI NAMIKANGO**

#### **A. SARE ZA SHULE**

##### **I. WASICHANA**

- i. Sketi jozi mbili ndefu yangi ya kijivu(ziwe na linda)
- ii. Shati mbili nyeupe mikono mifupi
- iii. Viatu vya ngozi jozi mbili rangi nyeusi viwe na visigino vifupi
- iv. Soksi ndefu nyeupe jozi mbili
- v. Sweta rangi ya bluu (blue) mikono mirefu. Itatumika wakati wa majira ya joto tuu
- vi. Kwa mtooa wa kike wa kiislamu kama atashona hijabu azingatie yafuatayo
  - ✓ Nusu kanzu inayofika usawa wa magoti
  - ✓ Sketi iwe ndefu na isiwe na linda
  - ✓ Hijabu iwe ndefu

##### **II. WAVULANA**

- i. Suruali jozi mbili za kijivu zenye linda mbili na mifuko mitatu
- ii. Shati nyeupe mikono mifupi jozi mbili
- iii. Viatu vya ngozi rangi nyeusi jozi mbili vyenye visigino vifupi (visiwe mabuti)
- iv. Soksi ndefu nyeupe jozi mbili
- v. Mkanda wa ngozi rangi nyeusi
- vi. Sweta rangi ya bluu (blue) mikono mirefu. Itatumika wakati wa majira ya joto tuu

#### **MUHIMU**

*Mzazi/mlezi kumbuka hatutampokea mwanafunzi ambaye atafanya maandalizi tofauti na fomu hii ya kujiunga inavyoelekeza*

#### **B. VIFAA VYA MICHEZO**

- i. Bukta na flana (shirt) jozi mbili rangi ya bluu (blue) kwa wavulana
- ii. Tracksuit na flana (shirt) rangi ya bluu (blue) jozi mbili kwa wavulana
- iii. Viatu vya michezo kama raba, njumu n.k

#### **MUHIMU**

*Mzazi/mlezi kumbuka michezo huirisha afya ya mwili na akili, hivyo michezo ni lazima kwa wote*

### **C. MAHITAJI YA DARASANI**

- i. Daftari kumi (10) aina ya (counter book quire three)
- ii. Mkebe (mathematical set), rula, penseli, peni, (kalamu ya wino)
- iii. Begi kwa ajili ya kubebea madaftari na vitabu (ni marufuku kutumia mifuko ya plastiki)
- iv. Dictionary ya oxford ENGLISH kwa KISWAHILI
- v. Kadi ya maendeleo
- vi. File kwa ajili ya kutunza kumbukumbu zake

### **D. MICHANGO YA CHAKULA**

- i. Mchele wa mahindi kg 20
- ii. Mboga (mbaazi, kunde, maharagw n.k)
- iii. Mafuta ya kula lit 1 yawe hayajafunguliwa (seal)
- iv. Vitunguu maji jagi 1
- v. Fedha tsh 10,000 malipo ya wapishi na gharama za kusagia yawekwe katika **ac no 70410003950 jina Namikango secondary Recurrent Account**

### **E. VIFAA VYA USAFI**

- i. Fagio la chelewa moja
- ii. Jembe moja likiwa na mpini wake
- iii. Kwanja moja

*Mzazi/mlezi kumbuka kuwa hatutapokea vifaa mtumba*

### **MUHIMU**

- i. Mwanafunzi aje na nakala ya cheti chake cha kuzliwa
- ii. Zoezi la kupima afya ni lazima lifanyike katika Hospitali ya Wilaya ya Nachingwea au katika Hospitali yeyote ya Serekali iliyokaribu nawe
- iii. Picha (passport size) moja yenye kivuli cha bluu

## **Kiambata namba 2**

### **SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebisha kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995.

Aidha, shule inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya ufundi yenye dhamana ya Elimu chini ya Ofisi Raisi TAMISEMI. Aidha, mwanafunzi anatakiwa kuzingatia kanuni zifuatazo kwa muda wote awapo shuleni na nje ya shule.

- a. Kuheshimu viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wenzake na jamii kwa ujumla
- b. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule
- c. Kuwahi kwa kufuata ratiba ya shule na katika shughuli nyingine atakazopewa
- d. Kufahamu mipaka ya shule na kuizingatia kikamilifu, kwa kupatiwa maelekezo juu kuwepo ndani na nje ya mipaka ya shule kwa kipindi chote.
- e. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule

### **MAKOSA YAFUATAYO YANAWENZA KUSABABISHA KUFUKUZWA SHULE AU KUSIMAMISHWA**

- i. Wizi
- ii. Uasherati, usagaji, ushoga na kuishi kimada
- iii. Ubakaji
- iv. Ulevi pombe na sigara, pia matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji wa bangi, cocaine, mirungi, n.k
- v. Kupigana, kupiga au kusababisha/kuchochea ugomvi
- vi. Kudharau bendera na wimbo wa taifa
- vii. Kuwa mjamzito, kutoa ujauzito au kusababisha mimba
- viii. Kuo au kuolewa
- ix. Kugoma, kuchochea/kuongoza na kushiriki mgomo
- x. Kukataa adhabu kwa makusudi
- xi. Kuwa na simu ya mkononi

**PRESIDENT'S OFFICE,  
REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**

**Namikango Secondary School  
P.O.BOX 115  
Nachingwea - Lindi**

REF: NO .....  
To The Medical Officers (District/regional)  
.....  
Sir/Madam,

**RE: REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION TO  
(Name of student).....**

Please examine the above named student and give the report regarding his/her suitability for undertaking secondary school studies.

1. Student's full name.....
2. Blood.....
3. Stool.....
4. T.B test .....
5. Syphilis test.....
6. Urine examination.....
7. Eyes test .....
8. Chest test.....
9. Ears test.....
10. Spleen.....
11. Abdomen.....
12. Pregnancy (for girls only).....

**ANY ADDITIONAL INFORMATION: EG Physical defects or impairment, infection, family diseases etc.**

.....  
.....

COMMENTS:.....  
.....

I certify that the above student is suitable/unsuitable for secondary school studies. If unsuitable give reasons

.....  
.....

**Name of Medical Officer** ..... **Signature** .....  
**Date** ..... **Official stamp** .....

## **A. YAH: KUKUBALI/KUKATAA NAFASI (MWAFUNZI)**

Mimi ..... nakiri kopokea barua ya kujiunga na masomo ya kidato cha kwanza katika shule ya Sekondari Namikango. Baada ya kusoma na kuelewa yaliyoandikwa katika fomu hii NIMEKUBALI NAFASI/NIMEKATAA NAFASI ya kuendelea na masomo.

Ninaahidi mbele ya mzazi/mlezi wangu kuwa nitazingatia kanuni, sheria na taratibu zote za shule. Kamwe sitoshiriki au kujihusisha na vitendo vya uvunjaji wa sheria za shule na makosa mengine ya jinai.

Nitatumia juhudi na maarifa katika kujifunza kwa manufaa yangu, wazazi, jamii na taifa kwa ujumla. Aidha niaahidi kuwepo shuleni muda wote wa masomo na endapo nitakuwa na udhuru wowote nitatoa taarifa kwa kuongozi wa shule kupitia kwa mzazi/mlezi

Jina la mwanafunzi .....saini .....tarehe.....

### **A. MAKUBALIANO YA MZAZI/MLEZI**

Mimi ..... Mzazi/mlezi wa mwanafunzi .....  
Wa kidato cha ..... mwaka ..... ninakubaliana na masharti tajwa hapo juu, hivyo naahidi kutekeleza mkataba huu na kuamuru mwanangu autekeleze. Endapo mwanangu atashindwa kutekeleza basi sheria ifuate mkondo wake. Aidha, niko tayari kufidia uharibifu wowote wa mali za shule utakaofanywa na mwanagu.

Jina la mzazi/mlezi .....saini.....tarehe.....